

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



TANGAZO

KUANZA KUTOA HUDUMA ZA KIUHAMIAJI UBALOZINI

Ubalozini unapenda kuwatangazia Watanzania wote waishio katika nchi za Nordic, Baltic na Ukraine kuwa umeanza tena kutoa kupokea maombi ya Pasipoti mpya za Kielektroniki na huduma nyinginezo za Kiuhamiaji kwa wenye mahitaji ambazo zilisimamishwa tangu tarehe 16/3/2020 kutokana na mlipuko wa ugonjwa wa Covid-19.

Hata hivyo, kwa kuwa tunatambua kwamba ugonjwa bado haujaisha kila mwombaji kabla ya kufika Ubalozini anatakiwa kuzingatia mambo yafuatayo:

- i. Maombi ya pasipoti na Hati ya dharura ya kusafiria yafanyike kwa njia ya mtandao kupitia www.immigration.go.tz ambapo baada ya kukamilisha taratibu zote muhimu mwombaji atawasiliana na Ubalozini kupitia barua pepe consular@tanemb.se au simu +4687322430 kwa ajili ya kupangiwa siku ya kufika Ubalozini kwa hatua zinazofuata.
- ii. Kila mwombaji azingatie kuwa taratibu za kujaza fomu za maombi ya Pasipoti hazifanyikii Ubalozini isipokuwa kila mmoja anatakiwa ajaze fomu yake kwa njia ya mtandao (www.immigration.go.tz) inayopatikana kwenye kipengere cha **e-services** na baada ya kukamilisha malipo ya dola 90 (\$ 90) awasiliane na Ubalozini.
- iii. Tunaendelea kuwasihi kwamba, pamoja na kuanza kutoa huduma za Kiuhamiaji lakini bado maambukizi ya Covid-19 hayajaisha, hivyo kila mmoja alipewa miadi ya kufika Ubalozini ahakikishe kuzingatia kanuni zote za Afya. Aidha, tunawashauri kila mmoja kufika Ubalozini siku aliyopangiwa ili kuepukana na msongamano Ofisini vinginevyo masuala mengine yasiyokuwa ya lazima kuja Ubalozini yamalizwe kwa njia ya barua pepe na simu.